# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI (102/2)**
**KIDATO CHA TATU**
**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**

**JULAI/AGOSTI 2025**

**SWALI 1: UFAHAMU (ALAMA 15)**

a)Kulingana na  mwandishi ni mambo gani ambayo yafaa tujitahadharishe nayo? (alama 3)

√Tujihadhari na hasira

√Tuepuke matumaini yaliozidi uhalisia

√Tuepuke ulevi wa ushindi

b)Tambua aina za elimu katika Maisha .(alama3)

√elimu ya kujielewa hao ni kina nani

√elimu ya kuturejeshea utu si elimu ya stashahada tunahitaji

√elemu ya maisha

c)Kulingana na taarifa ni mambo gani yanayochochea dhuluma katika jamii? (alama 4)

√umma kunyamaza na kukosa kutetea haki zao

√kushiriki katika uchaguzi wa viongaozi wabaya.

√Kukubali kunyanyaswa na viongozi dhalimu.

√Kumruhusu kiongozi katili kuendelea na ukatili kwa wananchi dhalili.

d)Ukirejelea kifungu hiki , (alama 2)

eleza maana ya ngoma ni lele.

√mwanzo wa jambo la kumtoa kiongozi mamlakani

e)Binadamu kamili ana sifa gani? (alama 1)

√Ni yule anayemwona mlemavu kama mwenzake

f)Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumika katika kifungu;

i)nikijihadaa nitafika mbinguni (alama 1)

√Kujidanganya kufanya jambo/ kukamilisha jambo

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

ii)Kumnyonyoa kipungu(alama 1)

√kumtoa kiongozi dhalimu uongozini

**SWALI 2: UFUPISHO (ALAMA 15)**

(i) Mambo muhimu katika kipengele hiki ni kwamba utungo wa ufupisho humhitaji mwanafunzi kueleza habari fulani kwa ufupi kadri iwezekanavyo, hasa kwa kuzingatia idadi ya maneno yanayohitajika

(ii) Mwanafunzi anahitajika kujieleza waziwazi kwa njia ambayo inaweza kueleweka vizuri na msomaji

(iii) Hoja zinatakiwa kupangwa kwa mtiririko na kwa njia ambayo itazifanya zionekane, zieleweke kwa urahisi na zikumbukwe pia.

(iv) Mtahiniwa azingatie ngeli kwenye nakala safi

(v) Azingatie idadi ya maneno pia

(vi) Matayarisho yaonekane waziwazi

(vii) Alama moja ya utiririko azawidiwe mtahiniwa mwenye makala bora.

**SWALI 3: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Kwa kutoa mifano mwafaka, fafanua dhana ya 'mzizi wa neno' (alama 2)

✓ Ni sehem ya neno isiyobadililabadilika katika hali mbalimbali

b) Andika sauti zenye sifa hizi. (alama 2)

i) Irabu ya mbele juu

✓/e/

ii) kipasuo ghuna cha kakaa laini

✓/g/

c) Tumia kivumishi cha pekee kisisitizi, nomino katika ngeli ya U-ZI kitunga sentensi (alama 2)

✓ Uzi wenyewe ulikatika

d) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. ( Alama 2)

N+V+E+T

√ Kitabu kizuri sana kilipotea

e) Bainisha maneno katika sentensi hii ( alama 2)

Karume ndiye mchezaji bora.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

✓N+t+N+V

f) Yakinisha,  (alama 2)

Askari wasiposhirikiana na raia wala kupiga doria hawatafaulu.

✓Askari wakishirikiana na raia na kupiga doria watafaulu

g) Tunga sentensi mbili kutofautisha maana ya neno (alama 4)

kucha

✓sehemu ya vidole

✓mwanafunzi atumie kucha kama kitenzi

h) Neno hili lipo katika ngeli gani ( alama 1)

Nyasi---------U-ZI

i) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa (alama 2)

Nyumba hizo zilijengwa mbali na mji ule.

✓Majumba hayo yalijengwa mbali na jiji lile.

j) Iandike sentensi upya katika hali ya kutendewa (alama 1)

Malik alipika uji.

✓Malik alipikiwa uji.

k) Tumia viwakilishi mwafaka badala ya maneno yaliyopigiwa mstari

Mtalii atazuru mbuga.

✓Yule atazuru ile

L)Andika kinyume cha sentensi ifuatayo.        (al 2)

Uduni ulifichika baada ya  kuanza kwa shughuli Ile

✓Ubora ulifichuka kabla ya kusitishwa kwa shughuli ile.

M)Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo        (al 3)

Ndege **yu** taabani ,japo **anajaribu** kujinasua

✓yu- t (kishirikishi kipungufu)

√anajaribu-Ts (kisaidizi)

√kujinasua- T (kikuu)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

N)Tumia kirejeshi amba- badala ya 'O' rejeshi katika sentensi ifuatayo (al 1)

Vazi lililonunuliwa limeruka

√Vazi ambalo lilinunuliwa limeraruka

O)Eleza maana za sentensi zifuatazo (al 2)

Mwandishi mwenyewe alituzwa

√ Dhana ya kusisitiza

Mwanafunzi mwenye hati nadhifu ni huyu

√Dhama ya umiliki

P)Tumia neno **mle** kama (al 2)

Kiwakilishi

√Mle mtafagiliwa

Kielezi

√Atafagia mle

Q)Ainisha viambishi . ( al 3)

Anayempikia

√√✓A-na-ye-m-pik-i-a

R) Fafanua maana ya neno kiimbo. (al 1)

√kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti katika uzungumzaji

S) Kamilisha jedwali lifuatalo. (al 4)

| Tendwa | Tendeka | Tendesha |
|---|---|---|
| Liwa | Lika | Lisha |
| Pakwa | Pakika | Pakisha |
| Katwa | Katika | Katisha |
| | | |

T) Sahihisha sentensi. (al 1)

Abiria walisafiri na ndege

√ Abiria walisafiri kwa ndege

**SWALI 4: ISIMU JAMII (Alama 10)**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Eleza maana ya istilahi hizi

i) lugha ya taifa

√Hutumiwa kama lugha bia katika nchi kwa ajili ya mawasiliano.

ii) lugha rasmi

√ Ni lugha inayotumiwa kutekeleza shughuli rasmi za nchi.

b) Eleza sifa za sajili ya maabadini/kanisani

√Hutumia msamiati wa kidini kama vile

Bibilia

maombi

mbinguni

jehanamu

Madhababu

Paradiso

Mbinguni

Mwenyezi Mungu

Mwokozi

√* Ni lugha inayonukuu sana hasa wazungumzaji wanaporejelea Kitabu kitakatifu

√Lugha yenye heshima, upole na unyenyekevu

√Lugha sanifu

√Ni lugha iliyojaa ahadi nyingi kwa wanaoandamana na mafunzo ya kidini na vitisho kwa wanaoenda kinyume na mafundisho

√Huwa imejaa matumaini

√Ni lugha yenye kutoa maneno ya sifa, kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu. (1X8=alama 8)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes